

Uzingativu wa Yaliyoandikwa kuhusu Mada: Mifano kutoka Baadhi ya Tasnifu za Kiswahili

*Samuel M. Obuchi
Chuo Kikuu cha Moi*

Ikisiri

Makala haya yanajadili nafasi ya yaliyoandikwa kuhusu mada katika taaluma ya utafiti. Mwandishi anarejelea data au kazi mbalimbali za kitafiti katika viwango vyatuzamili na uzamivu ili kutoa tahadhari kwa watafiti na wanataluma wanapokuwa mbioni katika kutekeleza majukumu ya kitafiti. Mwandishi yanajadili suala la mchango na manufaa ya utafiti kwa jamii hasa inapotokea kwamba utafiti unaohusika ni wa awali na haujawahi kufanywa na watafiti watangulizi. Makala yanajadili mustakabali wa utafiti katika taaluma za Kiswahili, huku akionyesha namna ya kujiepusha na changamoto zinazoendana na utafiti, katika mapana na marefu yake.

Maneno Muhimu: Yaliyoandikwa, Utafiti, Mada, Thamani ya Utafiti

Utangulizi

Makala haya yanajadili nafasi ya kipengele cha yaliyoandikwa kuhusu mada katika uandishi wa tasnifu katika kiwango cha uzamili na uzamivu. Mwandishi anaonyesha changamoto zinazowakumba waandishi na watafiti katika viwango hivi, huku akionyesha namna ambavyo watafiti wengi wameishia katika kuandika tasnifu zinazofanana. Hali hii hupelekea uandalizi wa tasnifu zisizotoa mchango wa thamani yoyote katika taaluma. Makala yamejadili nafasi ya kipengele cha yaliyoandikwa kuhusu mada, kwa mtafiti kama mwanajamii ambaye anahitajia kutangamana sio tu maandishi mbalimbali, bali pia na watafiti wanaokitwa katika eneo pana la utafiti fulani.

Pia tumerejelea matini mahususi ya kidini kwa lengo la kutilia mkazo umuhimu wa yaliyoandikwa kuhusu mada. Sehemu hii imesaidia katika kuonyesha kwamba yaliyoandikwa kuhusu mada ni kipengele cha utafiti kinachojitokeza katika taaluma mbalimbali zinazomhusu na kumzunguka mwanadamu. Kimsingi, makala haya yanajaribu kulifuatilia suala zima la makala kuwiana kutokana na ukweli kwamba watafiti hao wanapuuza maandishi au tafiti za awali zinazocukuana na tafiti zao. Hali hii imepelekea watafiti hao kuibuka na kazi ambazo, kwa kiasi kikubwa, zinaelekea kuwiana. Makala haya, basi yanalenga kueleza kwa kina nafasi ya yaliyoandikwa kuhusu mada katika mchakato mzima wa uandalizi wa kazi ya kitafiti. Katika makala haya,

nimerejelea mada mbalimbali zilizotokana na tasnifu mahususi. Hivyo, mjadala uliomo umekitwa kwenye hizo mada na maswali ya kihaipotheia, maswali ambayo pengine yatahitaji utafiti zaidi.

Msingi wa yaliyoandikwa kuhusu mada katika utafiti

Kipengele cha yaliyoandikwa kuhusu somo kimepewa umuhimu mkubwa katika taaluma ya uandishi. Kipengele hiki huwapa watafiti nafasi ya kuzitalii kazi mbalimbali ambazo zinahusiana na mada wanayoitafitia. Badala ya watafiti hawa kupitia kazi nyingi tu, ziwe tasnifu, vitabu, majarida na maandishi mengineyo, wao huishia kudhani kwamba mada wanayoitafitia haijashughulikiwa na watangulizi wao. Kuhusu nafasi ya kipengele hiki, Ponera (2019:42) anasema:

Mapitio ya maandiko ni kipengele kinachohusika na utafutwaji wa taarifa tangulizi kuhusiana na mada inayotafitiwa... Katika kila eneo au mada, tayari huwa kunakuwa na taarifa fulani kutoka kwa waandishi/watafiti wengine.

Maoni kama haya yanakuzwa na Mligo (2012) anayesema kuwa utafiti wowote unaotarajiwu kufanyika lazima ujengwe kwa kuzungukia tafiti zilizopita. Mtafiti apitie ripoti za tafiti nyingine pamoja na nyaraka mbalimbali kabla ya kuianza utafiti wake ili kuona kilichofanyika au kulibaini pengo la utafiti ambalo linafaa kuzibwa na utafiti mpya. Ukweli ni kwamba hii ni shughuli muhimu sana katika taaluma ya utafiti, ndiposa kuna rundo la maandishi kuhusiana na kipengele hili. Maandishi haya yanalenga katika kumuelekeza mtafiti katika kuhakikisha kwamba anaelewa fika kuhusu taratibu za kukusanya taarifa muhimu kuhusu kipengele anachokishughulikia.

Yaliyoandikwa kuhusu Mada: Msingi wa kifungu cha kidini

Ifahamike kwamba shughuli ya utafiti imepewa umuhimu mkubwa sio tu katika taaluma, bali pia katika shughuli nyinginezo za kimaisha. Yesu Kristo mwenyewe anatufundisha kuhusu nafasi ya yaliyoandikwa kuhusu mada kwa kuwarejelea Wafuasi au Mitume wake. Biblia Takatifu, katika Mathayo 16:13-17, tunaelezwa,

Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria-Filipi akawauliza wanafunzi wake, akasema, "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?" Wakasema, "Wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia, au mmojawapo wa manabii." Akawaambia, "Nanyi mwaninena kuwa mimi ni nani?" Simoni Petero akajibu akasema, "Wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai." Yesu akajibu, akamwambia, "Heri wewe Simoni Baryona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili bali Baba yangu aliye mbinguni.

Kifungu hiki kutoka Biblia kinatuelekeza kwenye kauli kwamba mapitio ya maandishi mbalimbali ni muhimu katika taaluma zote. Katika kifungu hiki, Yesu

mwenyewe anadhihirisha umuhimu wa yaliyoandikwa pale ambapo anawaauliza wanafunzi wake wampe taarifa walizo nazo kumhusu. Aliamini kuwa walikuwa na taarifa fulani kutokana na tajriba zao na maingiliano yao na wanadamu wenzao. Ndiposa kawaauliza wampe taarifa hizo. Hebu turejelee swalii lake:

Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?

Swali hili linachukuana na msingi wa yaliyoandikwa kuhusu mada, kwani huwa tunataka kuyafahamu wanayoyasema watafiti wengine kuhusu kipengele fulani tunachokitafitia. Katika kutekeleza hili, huwa tunarejelea vitabu, majarida, tasnifu na maandiko mengine. Ni kpitia kazi hizo na kutathmini mawazo yao huku tukipata mwanga wa kutosha kuhusu mbinu za kuchambua data, msingi wa utafiti ambaa utafaa zaidi katika utafiti wa sasa mionganii mwa mengine. Hapo ndipo tutafahamu ukweli ulioshamiri katika kazi hizo, huku tukitafakari kuhusu kipengele husika. Kwa kweli, tutakuwa tukijibu swalii: “Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?

Wanafunzi wa Yesu walihitajia kujibu swalii waliloulizwa. Wakamjibu:

Wakasema, “Wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia, au mmojawapo wa manabii.”

Kutokana na kifungu hiki, tunagundua kuwa wanafunzi walikuwa na taarifa muhimu kumhusu Yesu. Waliyafahamu waliyoyasema watu wengine. Taarifa hii ilimwezesha Yesu kujifahamu zaidi, hasa katika muktadha wa watu waliodhani kuwa walimjua. Majibu yao yalihitilafiana. Ndivyo hali ilivyo katika utafiti kwenye taaluma yoyote. Watafiti hawakubaliani kwa kila jambo. Kuna walioshughulikia kipengele fulani kwa kutumia data na nadharia fulani huku wakiyaandama malengo fulani mahususi. Katika kufanya hivi, wao huyafikia mahitimisho fulani ambayo si lazima yawiane. Hii ndiyo maana ya:...wengine hunena u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia, au mmojawapo wa manabii. Waliofikiri Yesu ni Yohana, walikuwa na sababu zao. Waliochukulia yeche ni Eliya, walielekezwa na pengine mfanano waliodhani ulikuwepo kati ya Yesu na Eliya. Hivi ni kusema kwamba kila mtafiti huwa na muelekeo wake anapoyashughulikia malengo yake ya utafiti. Mtafiti yejote mwenye uelewa wa matarajio ya utafiti wa kisayansi huhitajia kusoma kazi mbalimbali ili aweze kulimulika vizuri suala analoshughulikia, kiasi cha kuyajibu maswali ya utafiti. Usomaji wa kazi tangulizi humwezesha kupata mwanga wa kutosha kuhusiana na eneo zima la utafiti katika taaluma husika. Pasina kusoma kazi hizo, mtafiti huyo huenda akashughulikia yaliyokwishashughulikwa tayari. Matokeo yake ni kuwa atashindwa kutoa mchango wa kitaaluma. Baadaye, Yesu akawaauliza:

Nanyi mwaninena kuwa mimi ni nani?

Hapa, Yesu alitaka kuwa na uhakika kuwa wanafunzi wake, kwa kweli, walimfahamu barabara kama mwokozi wao. Kwa mantiki hii, mtafiti anafaa

kuwa na uhakika kuhusu kazi yake. Sauti yake inafaa kuchomoza katika utafiti wake. Anaporelea tafiti mbalimbali zilizotangulia, anafaa kutoa kauli yake kuhusu mada ambayo anaishughulikia. Hivyo, hafai kutupa orodha ya kazi ambazo amepitia. Anafaa kutoa kauli hakikifu kususiana na tafakuri yake. Ni kweli watangulizi wake walisema waliyoyasema, lakini ni muhimu zaidi kwa mtafiti kutoa mawazo na maoni yake. Ndiposa Yesu akawauliza: Nanyi mwaninena kuwa mimi ni nani?. Ajabu ni kwamba ni watafiti wengi hawazisomi kazi za watangulizi wao. Hivyo, hutokea kuwa hawana taarifa za kutosha kuhusu yaliyokwishakufanywa katika taaluma au eneo linalotafitiwa. Kutokana na kauli hii, ni bayana kwamba mtafiti hatarajiwi kutoa maelezo kikasuku. Anafaa kuyahakiki maandishi hayo kwa jicho la ndani. Hivyo, mtafiti anafaa kuzisaka taarifa hizo kutoka vyanzo mbalimbali: Majarida, magazeti, kamusi, Tasnifu, ensaiklopedia, vitabu. Mapitio ya maandishi ni muhimu sana katika mchakato wa utafiti kutokana na sababu zifuatazo:

- 1) Husaidia kujua ukomo wa watangulizi waliojishughulisha na eneo linalotafitiwa.
- 2) Humsaidia mtafiti kuthamini juhudzi za watangulizi wake: tayari lipo jambo fulani ambalo linafanyika; ni muhimu kutumia maarifa hayo ili kutambua jitihada hizo pamoja na kumsaidia mtafiti mpya kupata mwanga.
- 3) Huonyesha usayansi. Utafiti ni mchakato unaopaswa kufuata kaida maalumu: Kutafuta mawazo ya watafiti tangulizi ili kujihusisha na utafiti mpya.
- 4) Huwezesha kujua ukubwa/udogo/ugumu/urahisi wa kazi iliyo mbele.
- 5) Husaidia kulijua kwa kina eneo linalotakiwa kushughulikiwa.
- 6) Husaidia kufanyika kwa maandalizi ya namna zote (km. ya kifedha na ya kiakili) yanayotakiwa ili kuendesha zoezi ya utafiti.

Ponera ametoa hoja nzuri kuhusiana na umuhimu wa yaliyoandikwa. Ajabu iliyoko ni kwamba hapa Afrika Mashariki na kwingineko, shughuli hii haitiliwi maanani sana. Iliyo ni kwamba hoja hizi nzuri hazizingatiwi na wataalamu wengi katika shughuli za utafiti. Nchini Kenya, kwa mfano, kuna zaidi ya Vyuo Vikuu thelathini vya kitaifa na vingine vingi vya kibinafsi ambavyo hufundisha taaluma mbalimbali, Kiswahili kikiwemo. Utagundua kwamba vyuo hivi vingi vina wataalamu na watafiti wengi ambaao kwa kiasi fulani, si lazima washirikiane na wenzao kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali. Ni kutokana na hali hii ambapo watafiti na wasimamizi wao hutegemea rejea ndogo inayoweza kupatikana katika vyuo wanakofanyia utafiti wao. Hivyo, hujinyima nafasi ya kusoma maandishi mengineyo kando na kukosa kutagusana na wenzao katika eneo fulani la kitaaluma. Kwa mantiki hii, kuna uwezekano mkubwa kwamba wataalamu hao pia hujinyima nafasi ya kusoma kazi mbalimbali zilizowahi kuandikiwa fasihi, tafsiri, diskosi, isimu nk. Matokeo yake ni kwamba kazi hizo zinazotafitiwa

hukosa muktadha wa kitafiti, kando na uhondo na maarifa ya tafiti tangulizi. Ni kutokana na hali hii ambapo utagundua kwamba mwafulani ametafitia eneo fulani, kwa mfano; tafsiri, ila katika marejeleo yake, hakupata nafasi ya kusoma au kurejelea vigogo wanaotambulika katika taaluma hiyo. Hebu nitoe mfano: iwapo mwafulani nashughulikia taaluma ya sarufi maumbo, tunatarajia kwamba atakuwa amesoma kazi za upeo na matao ya juu kama vile Chomsky (1957, 1965). Ifahamike kwamba watahini wengi huanza kusoma tasnifu wanazotahini, wakianza na marejeleo. Baada ya kuititia sehemu ya marejeleo, mtahini huweza kuandaa kauli na mahitimisho yake ya mwanzo kuhusiana na kazi au tasnifu anayoisoma.

Kuna ushahidi kuwa watafifi wengi hawahimizwi kutembelea maktaba na vyumba vingine vyenye hifadhi kubwa ya rejea muhimu katika taaluma mbalimbali. Wasimamizi wengi kwa kweli ni watu wenye rundo la majukumu, hivi kwamba mara nyingi hawapati nafasi ya kusoma kazi nyingi tu, hata wanawapoelekeza wanafunzi wao katika uandishi wa tasnifu. Hali hiI hupelekeea uandalizi wa tasnifu ambazo, pengine si chapwa, ila zinakosa ule uhondo unaohusishwa na kazi tangulizi. Changamoto hii ingeepukwa iwapo watafifi hao wangekusanya taarifa nyingi zinazohusu yaliyokwishatafitiwa katika taaluma au eneo au mada fulani. Kuwa mantiki hii, kuna uwezekano wa mada moja kutafitiwa na wasomi au wanafunzi wengi. Vivyo, mtafiti au mtaalamu fulani anafaa kukusanya taarifa za kutosha kuhusiana na yaliyokwishafanywa na watafifi wengine kokote waliko duniani. Watafifi hao huweza kusemwa kuwa wanajuana kwa vilemba, kwani, wanaegemea nyanja na taaluma zinazokuza upamoja wao. Japo wasomi hao hawatakuwa wamekutana ana kwa ana, watakuwa wamejuana kimaandishi: Watakuwa wamesoma kazi za wenzi wao. Vinginevyo, kazi za kitafiti huiweza kusalia maktabani, hazisomwi na wengine. Hali hii huweza kutokana na baadhi ya wasomi kutotaka kutambuana. Hivyo, hawasomi kazi za wenzao; hawaamini kuwa wenzao wana uwezo wa kutafiti na pengine kuchapisha makala, vitabu na maandishi. Wao huishia kuzikashifu kazi hizo. Mtafiti aliyekomaa kimawazo hawezi kukashifu kazi yoyote iliyokwishachapishwa. Badala yake, huzisoma kazi hizo na kuziandikia makala, uhakiki na kadhalika kwa lengo la kuzipongeza au kuzikosoa kitaaluma. Mtafiti anfaa kujua kwamba utafiti wowote uliokushafanywa ni mchango wa aina fulani. Endapo kuna kasoro au kauli zinazoenda kinyume na imani, itikadi au kwa jumla zinazopingana na mantiki fulani, basi ana haki ya kuishughulikia katika makala yake.

Ni muhimu tufahamishe kwamba vyuo vikuu vingi haviwekezi kwenye vitabu na majorida, japo vinafunza na kuwaandaa wanafunzi katika viwango vya uzamili na uzamivu. Hata hivyo, watafifi na waelekezi wao wanafaa kuzisaka taarifa hizi kwenye mitandao na kwingineko. Vyuo vikuu hivi vingetekeleza wajibu muhimu wa kuhakikisha kwamba wanafunzi wa viwango mbalimbali

wanaosajiliwa humo wanapata rejea inayotosheleza mahitaji ya kazi zao. Aidha, Vyuo hivyo vitatarajiwa kuandaa orodha nzima ya mada za utafiti zilizokwishafanywa katika uwanja huo. Orodha hiyo itafaa kuhifadhiwa kwenye mtando wa Chuo hicho ambapo watafiti wengine watazisoma/watazirejelea. Hatua hii huenda ikapunguza uwezekano wa watafiti fulani kushughulikia mada zinazoelekea kuwiana.

- 1) Makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi katika shule za upili, Chuka!!
- 2) Makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi katika shule za upili mkoani Nyanza!!

Ukweli ni kuwa hamna ghala maalumu ambamo mtafiti atawezekana kupata mkusanyiko wa vitabu, hasa majorida. Ghala hilo lingempa mtafiti nafasi ya kuutambua tafiti zilizokwishafanywa. Aidha, hamna chombo ambacho kimetwika jukumu la kuziidhinisha mada zinazofaa au zinazoweza kutafitiwa. Ni kutoptera na mkondo huu wa mawazo ambapo tunaweza kubainisha nafasi ya yaliyoandikwa katika taaluma ya utafiti. Katika sehemu hii, mtafiti anafaa kuzingatia hoja zifuatazo katika kutekeleza na kukamilisha kazi yake ya utafiti:

- 1) Kulibainisha suala la utafiti linalofaa kushughulikiwa.
- 2) Kuziweka wazi mbinu za kitafiti zilizojaribiwa na watafiti tangulizi.
- 3) Kuonyesha namna mbinu hizo zilishindwa kutekeleza wajibu fulani ndiposa kukatokea haya ya utafiti huu kufanya.
- 4) Kueleza mbinu na mtazamo wako katika kulishughulikia suala hilo.
- 5) Kuonyesha msingi wa utafiti wako unaotokana na urejeleaji wa kazi au maandishi tangulizi.

“...You won’t reinvent the wheel and make it square...”

Tatizo, pengine, linaanza kwenye shughuli ya kuisaka mada ya utafiti. Mada husika inafaa kutafutiwa taarifa za kutosha. Mada hiyo isilandane na mada zilizokwishashughulikiwa. Hali hii huwezekana endapo mtafiti atasoma kazi nyingi za kitaaluma kuhusiana na eneo analopania kushughulikia.

Mapuuza ya watafiti katika kazi za Kitaaluma

Ilivyo ni kwamba watafiti wengi hawasomi kazi nyingi za kitaaluma mnamojadiliwa data mbalimbali kulingana na malengo na suala kuu lililouongoza utafiti fulani. Hivyo, huamua kushughulikia mada ambayo wanafikiri haijashughulikiwa. Mada inayofaa kushughulikiwa itakuelekeza kwenye tafiti mbalimbali kando na vitabu, majorida na ensaikolopidia. Hivyo, mtafiti atawezekana kuepuka mada isiyomwezesha kutoa mchango katika taaluma. Ni kutoptera na mantiki hii ambapo utawezekana mada maalumu inayopatikana baada ya kupitia maandishi mengi. Kinachonishangaza ni kuwa humu nchini, kuna tafiti mbalimbali ambazo, kwa kiasi kikubwa, zinalandana. Hebu angalia data ifuatayo:

- 1) Matatizo ya kisarufi mionganoni mwa wanafunzi wa kikipsigis wanaojifunza Kiswahili sanifu: mtazamo wa lugha kadirifu.
- 2) Makosa ya kisintaksia katika uandishi wa insha za Kiswahili za wanafunzi wa Kiswahili.
- 3) Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii.
- 4) Matumizi ya ngeli mionganoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya.
- 5) Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi na yanavyochangia matokeo mabaya ya mtihani, kata ya Ganze.
- 6) Uchanganuzi wa makosa katika insha za wanafunzi wa shule za upili: mfano wa wilaya ya Nakuru, Kenya.
- 7) Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na wanafunzi wa kitigania, Kenya.
- 8) Athari za kifonolojia kwa wasemaji wa dholuo wanaojifunza Kiswahili.
- 9) An analysis of errors in the written compositions of Trinidadian English Creole Speakers.
- 10) An analysis of lexical errors in the written English of standard eight pupils in Rigoma Division of Nyamira District.
- 11) An analysis of errors in Arabic Speakers English writings.
- 12) Athari za Ekegusii katika Kiswahili na zinavyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi wa Kisii wilayani Kisii Kusini.

Ukizichunguza mada zilizotajwa hapo juu kwa undani, utagundua kwamba zinaelekea kushughulikia mada ambazo, kwa kiasi kikubwa zinalandana. Nitatoa mifano:

1. Matatizo ya kisarufi mionganoni mwa wanafunzi wa kikipsigis wanaojifunza Kiswahili sanifu: mtazamo wa lugha kadirifu
2. Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi na yanavyochangia matokeo mabaya ya mtihani, kata ya Ganze.

Mada hizi mbili zinashughulikia mada ileile moja: matatizo/makosa ya kisarufi! Maeneo yab utafiti ndiyo yanatofautiana. Iwapo watafiti hawa wawili wangechunguza maandishi mbalimbali, pasina shaka, wangeziandaa mada zao upya, zisije zikalandana. Ni kutokana na hali hii ambapo tunajiuliza: je, kazi hizi zinazolandana zinatoa mchango gani katika taaluma? Pengine zinatofautiana kwa kiwango fulani, ila msomaji huenda akafikiri kuwa kazi moja ni kivuli cha kazi nyininge. Tupate mfano mwininge:

3. An analysis of **lexical errors** in the written English of standard eight pupils in Rigoma Division of Nyamira District.

4. An analysis of errors in Arabic Speakers English writings.

Kazi hizi mbili zilizotajwa hapo juu zinashughulikia mada ileile moja: **makosa!** Hatuna uhakika iwapo kazi hizi zinatofautiana kiuhakiki. Zinaelekea kutofautiana pale ambapo mmoja anarejelea data iliyoko eneo fulani nchini Kenya. Mwingine anarejelea data ya kiarabu. Aidha, hatuna uhakika ikiwa kazi hizi mbili zinatofautiana tunaporejelea yaliyomo. Kilichoko ni kwamba mada hizi hazikupaswa kulandana. Mmoja anashughulikia makosa kwa ujumla. Mwenzake anarejela makosa ya kisarufi. Kuna uwezekano mkubwa kwamba aliyeshughulikia makosa kwa ujumla aliangalia pia makosa ya kisarufi mionganoni mwa makosa mengine. Ndipo tunashindwa kuelewa kwa nini wao wawili wakashughulikia kipengele kilekile. Tupate mfano mwingine hapa chini:

5. Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na wanafunzi wa kitigania, Kenya
6. Athari za Ekegusii katika Kiswahili na zinavyochangia matokeo mabaya ya mtihani wa kitaifa wa Kiswahili kwa wanafunzi wa Kisii wilayani Kisii Kusini.

Ukiziangalia mada hizi mbili, utagundua kuwa zinazungumzia kipengele: *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru.../ Athari za Ekegusii katika Kiswahili...!*

Kwa ufupi, ni wazi kuwa watafiti wengi wameshindwa kujikita kwenye nidhamu ya kitafiti. Mtafiti ambaye anaandaa tasnifu yake kwa ajili ya mahitaji fulani, anafaa kuwa na uhakika kuhusu suala kuu linalouongoza utafiti wake huku akiongozwa na malengo mahususi. Ili kupata mada inayofaa na ambayo haijawahi kuandikiwa, mtafiti anafaa kuzitalii tafiti mbalimbali. Katika kufanya hivyo, atapata orodha ya kazi hizo. Hatua ya kwanza ni kuhakikisha anaripoti, kwa ufupi sana, yaliyomo katika kazi hizo, kando na kuonyesha namna kazi hizo zilimfaidi katika utafiti wake. Hivi ni kusema kwamba mtafiti anafaa kuiripoti kweli inayodhiri katika kazi yake ya utafiti. Ukweli na uhakikifu huu hutokana sio tu na uchambuzi wa data iliyokusanywa, bali pia na muumano uliopo kati ya utafiti wako na tafiti zilizotangulia. Kwa njia hii, mtafiti huweza kutupilia mbali kiasi fulani cha data ambacho, pengine, inatokana na tafiti tangulizi, data ambayo haiendani na malengo na mahitaji ya utafiti wake. Mtafiti, pia, anaweza kuutambua ufilisi wa msingi wa kinadharia uliotumiwa na watafiti tangulizi. Msingi wowote wa kiandharia unafaa kutosheleza majukumu kadhaa.

Kwanza, kuna Msingi wa kiumilisi. Hapa, mtafiti anafaa kuwa na uelewa mpana wa mijadala mikuu inayojitekeza katika taaluma au mada anayoishughulikia, ikiwa ni pamoja na mafanikio, michango na mitafaruku ambayo imetokea katika eneo hilo. Katika kufanya hivi, mtafiti atakuwa anakuza hoja kwamba amepata mwanya au pengo ambalo halikushughulikiwa na tafiti tangulizi, na kwamba atakuwa na usemi au kauli fulani kuhusu mjadala

unaoendelea. Mtafiti, basi, anatarajiwa kuuendesha utafiti wake kitaaluma kwa kuyahakiki maandishi mbalimbali, kwa jicho la ndani.

Pili, kuna Msingi wa ulengaji. Msingi huu huweka wazi kipengele kinachoangaliwa. Hapa, mtafiti huliweka wazi suala la utafiti, malengo na nadharia tete ya utafiti, pamoja na kuifua tilia mijadala na mitafaruku inayoshamiri katika eneo hilo la utafiti. Mtafiti, akiongozwa na msingi huu huweza kuonyesha namna anavyochoambua data mahususi katika kuyafikia mahitimisho yanayokubalika. Hivi ni kusema, mtafiti anatarajiwa kuhakikisha kwamba anaongozwa na dira maalumu katika kuunganisha, kulinganisha, kufuatanisha na kuvioanisha vipengele mbalimbali vya utafiti au tasnifu. Kwa kutumia msingi huu, mtafiti anafaa kuhakikisha kwamba anatumia data inayofaa na kutosheleza mahitaji ya tasnifu au utafiti.

Mwisho, mtafiti anafaa kutegemea msingi wa data. Data hutumiwa kama ushahidi kuhusu mtazamo, maoni, kauli na hoja zinazokuzwa katika utafiti unaohusika. Kwa njia hii, tunaweza kutoa kauli za hakika kuhusu kipengele fulani, kwani, tutakuwa tunachangia taaluma fulani. Hivi ni kusema, msingi wa kinadharia hutuwezesha kuhakikisha kwamba data inayotumiwa katika kuianda tasnifu fulani inafaa na inatosheleza mahitaji na malengo ya kazi husika. Kauli na mijadala inayozuka katika kazi husika inafaa kutegemezwu kwenye data mahususi ambayo inafaa kuambatanishwa mwishoni mwa utasnifu. kwa mantiki hii, mtafiti atawenza kuziepuka mbinu na nadharia hizo pungufu.

Iwapo watafiti wa kazi zilizotakwa hapo juu wangezingatia hili, pasina shaka, wangeandaa mada zinazotafautiana. Ni kutokana na maelezo haya ambapo tunafaa kukumbuka kwamba *yaliyoandikwa kuhusu mada* huliweka wazi suala la utafiti na kuzibainisha mbinu zilizotumiwa na watafiti tangulizi. Ifahamike kwamba utafiti hautekelezwi kwenye ombwe tupu. Utafiti unaofanyika leo unafaa kuegemezwu kwenye utafiti uliotangulia, ndiposa kazi tangulizi zinakuwa kama dira na mwongozo unaomwezesha mtafiti wa sasa kuyamulika masuala fulani yanayohusu utafiti wake. Baada ya kuzipitia kazi tangulizi, mtafiti atawenza kudhihirisha mtazamo wake kuhusu suala ambalo linashughulikiwa. Kwa ufupi, mtafiti anafaa kuuingiza utafiti wake kwenye muktadha wa tafiti tangulizi. Maxwell (2005) anatoa orodha ya hoja za kuzingatiwa katika kuhakikisha kuwa kazi fulani ya kitafiti inakubalika kindakindaki:

- i. Mtafiti anafaa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya pendekemo la utafiti, hasa kuhusiana na ukusanyaji na uchambuzi wa data. Hapo, atapata nafasi ya kuutathmini msingi wa kinadharia, kutangamana na maandishi ya watafiti wenza kwa lengo la kupata mwanga mpya kuhusu taaluma anayoishughulikia (Backer 1970).
- ii. Mapitio ya stakabadhi, nyaraka na maandishi mbalimbali humwezesha mtafiti kukusanya data inayofaa na inayotosheleza mahitaji ya malengo

- ya utafiti wake (Emerson, Freetz na Shaw, 1995). Data hii humwezesha mtafiti kuyafikia mahitimisho yanayokubalika.
- iii. Haja ya kuhakikisha ufaafu wa data kwa kuwahusisha watafitiwa, watafiti wenza na wengine wanaoweza kutoa taarifa muhimu na ya msingi kuhusu maana na vijisehemu nya data, kwa lengo la kufungia nje mapendeleo ya mtafiti. Bila shaka, hii ni hatua nzuri katika taaluma ya utafiti kwani humwezesha mtafiti kupata maelezo fulani kuhusu yanayoendelea katika taaluma pana anayoishughulikia.
 - iv. Mtafiti hutarajiwu kujitosa nyanjani ambamo hujionea kinachoendelea kule kuhusiana na vipengele anavyovishughulikia. Hivyo, atapata mwanga wa kutosha, hasa anapogundua kuwa watafiti wenza hawakukusanya data iliyotosha, au pengine walitoa maana ya vipengele fulani nje ya muktadha. Ni kwa mantiki hii ambapo ataweza kuyatambua mapungufu yanayoendana ya tafiti tangulizi (Huberman 1994).
 - v. Baada ya kuzihakiki tafiti mbalimbali, mtafiti ataweza kuichunguza upya data aliyokusanya na kutupilia mbali vijisehemu nya data visivyoendana na malengo yake ya utafiti. Bila shaka, atakuwa amepata tahadhari fulani na kazi hizo alizopitia.
 - vi. Mtafiti anafaa kusaka taarifa kutoka kwa watu mbalimbali, kuitia vitabu, majarida, tasnifu na maandiko mbalimbali. Aidha, mtafiti anaweza kuwahoji watafiti na watu maarufu katika taaluma husika. Hivyo, ataweza kuzigundua dosari mbalimbali zinazojitokeza katika tafiti hizo za awali, na kuandama njia na maarifa ya kuzipunguza changamoto hizo. Hali hii huenda ikapekelea upatikanaji wa kazi yenye thamani kubwa.
 - vii. Mtafiti anafaa kutumia kiasi kikubwa cha data katika kuziendeza hoja zake. Kuna uwezekano kuwa tafiti tangulizi hazikuzingatia data ya kutosha. Mapitio ya kazi hizo ni nafasi nzuri ya kugundua namna ya kuepkana na utafiti chapwa na usiofaa.
 - viii. Mapitio ya maandishi mbalimbali humwezesha mtafiti kuinganisha kazi yake na tafiti tangulizi. Njia itamwezesha kutambua chimbuko la suala au kipengele cha utafiti, hali ambayo itamwezesha kuhakikisha kuwa anatumia mbinu zinazofaa sio tu za kukusanya data, bali pia taratibu mwafaka za kuichanganua data kulingana na suala la utafiti na malengo yanayouongoza utafiti.

Mustakabali wa utafiti katika taluma ya Kiswahili

Tujiulize, kwa nini tunashiriki uchunguzi wa utafiti katika taaluma, hususan Kiswahili? Utafiti wowote unafaa kufanyika ili uwe mchango katika taaluma husika. Katika kufanya hivyo, tunatarajiwu kuibua maswali ya kimsingi, kuandama malengo mahususi na kulifuatilia suala kuu linalopaswa kutafitiwa na

kutanzuliwa. Hivyo, tunafaa kusoma maandishi mbalimbali ya kitafiti kwa nia ya kupata mwelekeo kuhusiana na mapengo yaliyo wazi na yanayofaa kujazwa kupidia ukusanyaji na uchambuzi wa data mahususi. Kwa kurejelea watafiti wengineo, mtafiti ataweza kutambua njia mwafaka za kukusanya data ya aina fulani kutegemea malengo yanayouongoza utafiti wake. Data tuliyoirejelea hapa inabainisha kauli kwamba pengine wasomi na watafiti fulani hawarejelei na wala hawasomi yaliyoandikwa na wengine. Bila shaka, huu ni mwelekeo unaoweza kushamiri na kuangamiza moyo na roho ya utafiti. Utafiti wowote unafaa kujengeka kwenye muktadha wa tafiti zilizotangulia. Usomaji wa kazi zilizotangulia humwezesha mtafiti yejote kuuimarisha utafiti wake; ukweli ni kuwa mtafiti yejote hafai kudhani kuwa eneo au kipengele fulani hakijashughulikiwa na watangulizi wake. Tafiti zilizotangulia zitampa nafasi ya kupata mwanga, mwelekeo na dira kuhusiana na namna ya kukabiliana na kipengele fulani, kando na kumpa misingi ya kuichambua data husika ili kufikia kauli au mahitimisho fulani yanayokubalika. Pasina kurejelea maandishi mbalimbali, huenda watafiti wengi wakatafitia mada zilizokwishashughulikiwa na watangulizi. Basi, utaepuka mada zilizoshughulikiwa, malengo yaliyoandamwa na kufikiwa, na kuzifahamu mbinu mwafaka za kushughulikia utafiti husika.

Utafiti ni shughuli ya kisayansi kwa maana kwamba mtafiti anatarajiwa kufuata taratibu za kisayansi katika kuandaa malengo mahususi na kufuata makini fulani katika kukusanya data itakayomwezesha kufikia mahitimisho fulani. Mtafiti, basi, atatarajiwa kuichambua data fulani, ama inayopatikana nyanjani au kwenye matini ya kifasihi. Hivyo basi, mtafiti aliye na makini fulani hataweza kutafitia mada zilizoshughulikiwa wala kutumia mbinu na njia potovu ambazo, pengine, zilipuuziliwa mbali na watafiti tangulizi. Kwa mantiki hii, mtafiti aliye makini atafuatu mbinu, njia na taratibu zinazokubalika katika kuutekeleza wajibu wake. Inapotokea kuwa watafiti fulani wamejitekeza na mada ileile moja inayokitwa kwenye data ileile, basi hapo kuna hatari ya kurudia kikasuku yale yaliyokwishafanywa. Ifahamike kuwa utafiti uliojengeka kwenye misingi ya kisayansi hutarajiwa kutanzua suala fulani la kitafiti na matokeo yatachangia katika kuliziba pengo fulani la kiakademia. Mtafiti anaposhughulikia mada amabyo, tayari, ishashughulikiwa, atakuwa hatoi mchango wowote wa kitaaluma, na hivyo, atashindwa kuziba pengo lolote.

Hitimisho

Kuna haja ya watafiti kusoma kazi za watafiti tangulizi kwa faiada yao wenye kama watafiti. Usomaji huu utawawezesha kuzitambua tafiti mbalimbali zilizokwishafanya katika eneo linaloshughulikiwa, na hatua hii itamwezesha mtafiti kuhakikisha kwamba anaepuka mada ambazo tayari zimetafitiwa. Iwapo mtafiti atashindwa kuyapitia maandishi ya watangulizi wake, basi huenda

akafikiri kuwa mada fulani haijashughulikiwa; kuna uwezekano mkubwa kwamba baada ya utafiti wake kukamilika, atagundua kuwa hana pengo la kujaza; pengo hilo lilishajazwa na watangulizi wake.

Marejeleo

- Emerson R. M., Freetz R. I. & Shaw L. L. (1995). *Writing Ethnographic Footnotes*. Chicago: University of Chicago Press.
- Backer H. S. (1970). *Sociological Work: Methods and Substance*. Chicago: Aldine.
- Biblia Takatifu. (1984). Grand Rapids: Zondervan Publishing House.
- Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures*. The Hague: Mouton.
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: MIT Press.
- Maxwell J. A. (2005). *Qualitative Research Design: An Integrative Approach*. United Kingdom: Sage publications Limited.
- Mligo E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: mwongozo kuhusu utafiti na uandishi wa ripoti yenye mantiki*. Dar: Ecumenical Gathering.
- Ponera A. S. (2019). *Misingi ua Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Ruane J. M. (2005). *Essentials of Research Methods: A guide to Social Science Research*. Oxford: Blackwell Publishing.
- Laws P., Harper C., & Marcus R. (2003). *Research for Development: A Practical Guide*. New Delhi: Vistaar Publications.